TANGAZO LA SERIKALI NA. 448 la tarehe 07/6/2024

SHERIA YA MISITU
(SURA YA 323)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 29(1))*

AMRI YA KUTANGAZA MSITU WA HIFADHI YA MAZINGIRA ASILIA VIKINDU YA MWAKA 2024

## UTANGULIZI

KWA KUWA, misitu ya hifadhi ya Pugu, Kazimzumbwi na Vikindu ilikusudiwa kutangazwa kama msitu mmoja wa Hifadhi ya Mazingira Asilia Pugu-Kazimzumbwi kwa mujibu wa TS. Na. 190 la 2020;

NA KWA KUWA, kwa mamlaka niliyonayo kama Waziri mwenye dhamana ya Maliasili na Utalii, kwa mujibu wa kifungu cha 29(1) cha Sheria ya Misitu Sura ya 323, kwa maslahi ya Umma na Taifa kwa ujumla nimeona ni vema kutangaza Msitu wa Hifadhi ya Mazingira Asilia Vikindu;

KATIKA MUKTADHA HUO, Amri hii inabainisha yafuatayo:

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Kutangaza Msitu wa Hifadhi ya Mazingira Asilia Vikindu ya mwaka 2024.

Tangazo

2. Eneo la Msitu wa Hifadhi Vikindu ndani ya mipaka iliyoainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa Msitu wa Hifadhi ya Mazingira Asilia Vikindu.

JEDWALI


WILAYA YA MKURANGA

MSITU WA MAZINGIRA ASILIA VIKINDU

*Eneo:* Hekta 1668 au kilometa za mraba 16.68 Unakopatikana na Mipaka Eneo lote la Msitu wa Hifadhi Vikindu uliopo katika Wilaya ya Mkuranga, Mkoa wa Pwani kwa kadiri inavyobainishwa katika Ramani Jb 3133 ya mwaka 2022 (Skeli 1:20000) lenye ukubwa wa hekta 1668 au kilometa za mraba

*Tangazo La Serikali Na. 448 (Linaendelea)*

16.68 ambao ramani yake imehifadhiwa na Mkurugenzi wa Upimaji cha Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, na lenye mipaka ifuatayo:




| | |
|---|---|
| Dodoma, | ANGELLAH JASMINE KAIRUKI |
| ___24 Mei, 2024 | *Waziri wa Maliasili na Utalii* |